JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA KILIMO
# BODI YA KOROSHO TANZANIA



# JARIDA LA MWEZI
## Machi 2024.

Toleo Jipya

#KilimoBiashara

## 1.0 UTANGULIZI

Msimu wa Korosho nchini Tanzania huanza mwezi Oktoba na kuisha mwezi wa Aprili, hii ni baada ya Mikoa mipya kuanza kuzalisha korosho. Hata hivyo zaidi ya asilimia 90 ya korosho ghafi huzalishwa katika mikoa ya kusini mwa Tanzania ambayo ni Mtwara, Lindi, Ruvuma na Pwani ambayo msimu wake ni kuanzia Oktoba hadi Mwezi Januari. Mpaka sasa minada katika mikoa hiyo tayari imesitishwa. Kiasi kidogo cha korosho zilizobaki kwa wakulima zinaendelea kuuzwa kwa wabanguaji wa ndani kupitia Soko la awali. Kwa upande wa kanda ya Kaskazini na kanda ya kati, hususani mikoa ya Tanga, Dodoma na Singida mavuno huanza mwezi wa Februari hadi Aprili lakini kutokana na kukithiri kwa mvua mavuno ya korosho kwa kanda hii yamechelewa kuanza, hivyo mpaka sasa hakuna mkoa wa kanda hizo ulioanza kufanya minada kama ilivyozoeleka kwa misimu mingine.



## 2.0. MWENENDO WA SOKO LA KOROSHO KATIKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI MWEZI FEBRUARI, 2024.

### 2.1. MWENENDO WA SOKO AFRIKA MAGHARIBI

Nchini Ivory Coast kumekuwa na ongezeko la mauzo ya korosho ghafi sokoni wakati wa karibu na sikukuu ya Pasaka. Masafirisho ya korosho nje ya nchi yameanza rasmi lakini upandaji wa bei uliokuwa unasubiriwa kwa muda mrefu haujafanikiwa. Ubora wa korosho umeshuka (kwa sasa ni ratili 46 na 47) kutokana mvua kubwa iliyoanza kunyesha kuanzia katikati ya mwezi Machi. Bei ya korosho ghafi katika ngazi ya mkulima ni kati ya Dola za Kimarekani 0.45 hadi 0.54 (Shilingi 1,154 hadi 1,385) kwa kilo.
Msimu uliopita Ivory Coast ilibangua kiasi cha tani 265,863 za korosho ghafi na kusafirisha nje ya nchi tani 50,200 za korosho karanga.
**Chanzo:** African Cashew Alliance

Kwa upande wa nchi ya Ghana wanunuzi wamepunguza kasi ya ununuzi wa korosho tofauti na wiki mbili za mwanzo za mwezi Machi. Wadau wanafikiri ni njama inatumika ili kulazimisha bei kushuka kwa kutengeneza mazingira ya usambazaji uwe mkubwa sokoni tofauti na mahitaji, lakini ukweli ni kwamba mavuno ya kwanza yameisha na mavuno ya pili yanatarajiwa kuanza hivi karibuni. Bei ya korosho ghafi katika ngazi ya mkulima ni kati ya Dola za Kimarekani 0.45 hadi 0.68 (Shilingi 1,154 hadi 1,744) kwa kilo ubora ukiwa ni ratili 48 na 50 (48-50lbs).
**Chanzo:** African Cashew Alliance na Nkalo

Nchini Nigeria mauzo ya korosho ghafi yanaendelea huku wiki ya mwisho ya mwezi Machi ikishuhudiwa kushuka kwa bei kutokana na kushuka kwa kiwango cha kubadilisha fedha za kigeni. Ubora wa korosho bado ni mzuri, bei ya korosho ghafi katika ngazi ya mkulima ni kati ya Dola za Kimarekani 0.58 hadi 0.69 (Shilingi 1,488 hadi 1,770) kwa kilo ubora ukiwa ni ratili 48 na 52 (48-52lbs).
**Chanzo:** African Cashew Alliance

Kwa upande wa Benin Bei ya korosho ghafi katika ngazi ya mkulima ni kati ya Dola za Kimarekani 0.50 hadi 0.58 (Shilingi 1,283 hadi 1,488) kwa kilo. Serikari ya Benin imezuia usafirishaji wa korosho nje ya nchi kuanzia Aprili Mosi, 2024, wasafirishaji wa korosho ghafi kwenda nje ya nchi watahitaji kuthibitishwa na Waziri wa biashara. **Chanzo:** African Cashew Alliance na Nkalo

## 2.2. Hali ya Soko la Korosho Nchini India

Nchini India msimu wa mauzo wa korosho ghafi kwa soko la ndani umeanza rasmi katika miji ya Goa, Maharashtra na Kankavli, bei ikiwa ni kati ya Dola za Kimarekani 1.33 hadi 1.42 (Shilingi 3,411 hadi 3,642) kwa kilo ubora ukiwa ratili 52 hadi 53 (52-53lbs). Mavuno yanatarajiwa kuwa machache kutokana na hali ya hewa ya joto na baridi kidogo wakati wa msimu. Bei ya korosho inayoagizwa kutoka nchi za Afrika kwa mwezi Machi ni kati ya Dola za Kimarekani 970 hadi 1,060 kwa tani (CIF-India) kwa ubora wa Ratili 46 hadi 49.
Soko la ndani la korosho karanga linaendelea kuwa ndaifu ila linatarajiwa kuimarika taratibu katika wiki chache zijazo.
Chanzo: Cashewnut information

## 2.3. Hali ya Soko la Korosho katika Nchi ya Vietnam

Nchini Vietnam soko la korosho ghafi bado limeendelea kuwa thabiti, huku bei ikiendelea kupanda. Taarifa mbalimbali zinaeleza ya kwamba korosho kutoka Afrika Magharibi ni chache na zenye ubora wa chini kutokana na kukithiri kwa mvua za El Nino. Bei ya korosho ghafi kutoka Afrika ni kati ya Dola za kimarekani 1,040 hadi 1,065 (CNF-Vietnam) kwa tani kwa ubora wa Ratili kati ya 47 (lbs) hadi 48 (lbs).
Chanzo: Cashewnutinformation

**Jedwali Na. 1 Tathmini ya Uzalishaji wa Korosho kwa Nchi za Afrika Magharibi kwa Misimu ya 2022/2023 na 2023/2024**


| NCHI | UZALISHAJI KOROSHO GHAFI (TANI) | | | NCHI ZILIKOUZWA 2023 (TANI) | | | | KIASI KILICHOBANGULIWA NDANI YA NCHI (TANI) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2022 | 2023 | 2023 VS 2022 | Vietnam | India | China | Nchi Nyingine | 2022 | 2023 | 2023 VS 2022 |
| Ivory Coast | 1,150,000 | 1,503,375 | ▲30.7% | 899,430 | 190,945 | | 3,000 | 179,000 | 265,000 | ▲48.0% |
| Ghana | 190,000 | 223,758 | ▲17.8% | 259,320 | 216,124 | 2314 | | 10,000 | 16,000 | ▲60.0% |
| Burkina Faso | 155,000 | 188,500 | ▲21.6% | 35,000 | 40,500 | | | 17,000 | 18,000 | ▲5.9% |
| Mali | 90,000 | 105,761 | ▲17.5% | 700 | 311 | 750 | 3,000 | 800 | 1,000 | ▲25.0% |
| Togo | 35,000 | 41,569 | ▲18.8% | 35,000 | 165,174 | 2395 | | 5,000 | 4,000 | ▼20.0% |
| Nigeria | 345,000 | 418,690 | ▲21.4% | 266,781 | 81,909 | | | 78,000 | 70,000 | ▼10.3% |
| Benin | 195,000 | 240,429 | ▲23.3% | 20,000 | 108,016 | 2413 | | 10,000 | 15,000 | ▲50.0% |
| Guinea | 100,000 | 120,199 | ▲20.2% | 60,000 | 79,199 | | | 500 | 1,000 | ▲100.0% |
| Guinea Bissau | 270,000 | 276,622 | ▲2.5% | 95,000 | 56,622 | | | 4,000 | 5,000 | ▲25.0% |
| Senegal | 67,000 | 69,411 | ▲3.6% | 80,000 | 81,911 | | | 1,600 | 2,500 | ▲56.3% |
| Gambia | 26,000 | 28,662 | ▲10.2% | 13,000 | 20,162 | | | 500 | 500 | ▶0.0% |
| JUMLA | 2,623,000 | 3,216,976 | ▲22.6% | 1,764,231 | 1,040,873 | 7,872 | 6,000 | 306,400 | 398,000 | ▲29.9% |

**Chanzo:** Cashewnutinformatio

## Jedwali Na 2:Bei za Korosho Ghafi Katika Nchi ya India na Vietnam Februari, 2024

| MWENENDO WA BEI ZA WASTANI ZA KOROSHO GHAFI DUNIANI INDIA NA VIETNAM KWA KIPINDI CHA JANUARI 2023 HADI FEBRUARI 2024 | | |
|---|---|---|
| TARAHE | Bei - CIF USD / TON | |
| | BEI YA CHINI | BEI YA JUU |
| 18 Februari, 2023 | 1,180 | 1,230 |
| 13 Machi, 2023 | 1,150 | 1,165 |
| 24 April, 2023 | 1,040 | 1,080 |
| 20 Mei, 2023 | 1,040 | 1,130 |
| 18 Juni, 2023 | 925 | 1,065 |
| 22 Julai, 2023 | 925 | 1,080 |
| 21 Agosti, 2023 | 950 | 1,080 |
| 23 Septemba, 2023 | 1,030 | 1,165 |
| 16 Octoba, 2023 | 1,030 | 1,165 |
| 25 November, 2023 | 1,180 | 1,230 |
| 26 Desemba, 2023 | 1,080 | 1,190 |
| 14 Januari, 2024 | 1,060 | 1,100 |
| 24 Februari, 2024 | 1,040 | 1,150 |
| 30 Machi, 2024 | 1,040 | 1,065 |
| SOT: 46-48 | | |

**Chanzo:** Cashewnutinformatio




**Chanzo:** Cashewnutinformatio

## 3.0 BEI ZA KOROSHO KARANGA KUTOKA NCHI MBALIMBALI DUNI

Bei ya korosho karanga katika nchi mbalimbali hutofautiana kwa kuzingatia kiwango cha uzalishaji, gharama za uzalishaji, viwango vya ubora pamoja na teknolojia inayotumika kubangua korosho ghafi.

### 3.1 Bei ya Korosho Karanga Vietnam Kufikia FEBRUARI, 2024

Nchini Vietnam bei ya korosho karanga iko chini kidogo ikilinganishwa na bei katika nchi zingine zinazobangua korosho. Kuna mabadiliko ya bei kwa mwezi Machi kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 3

**Jedwali Na. 3: Bei za Korosho Karanga Nchini Vietnam hadi kufikia Machi, 2024**

| BEI YA KOROSHO KARANGA VIETNAM HADI KUFIKIA MACHI, 2024 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAUZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Juu | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | 180 WW | 7.39 | 7.61 | 18,955.35 | 19,519.65 |
| White Whole Cashews 210 | WW 210 | 6.50 | 6.62 | 16,672.50 | 16,980.30 |
| White Whole Cashews 240 | WW240 | 5.78 | 6.06 | 14,697.45 | 15,543.90 |
| White Whole Cashews 320 | WW320 | 5.03 | 5.403 | 12,901.95 | 13,851.00 |
| Large Pieces | LP | 3.26 | 3.53 | 8,361.90 | 9,054.45 |
| Small Pieces | SP | 1.98 | 2.21 | 5,078.70 | 5,668.65 |

**Chanzo:** Cashewinformation

### 3.2 Bei ya Korosho Karanga katika nchi za Afrika Magharibi Hadi Kufikia Machi, 2024

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari, bei ya korosho karanga kwa nchi za Afrika Magharibi ambazo ni Ivory Coast, Ghana, Benin nk. Inakadiriwa kuwa kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 4

**Jedwali Na. 4: Bei ya Korosho Karanga Afrika Magharibi hadi Kufikia Machi, 2024**

| BEI YA KOROSHO KARANGA AFRIKA MAGHARIBI HADI KUFIKIA MACHI, 2024 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | W180 | | | | |
| White Whole Cashews 180 | W210 | 7.27 | 7.50 | 18,647.55 | 19,237.50 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 5.95 | 6.17 | 15,261.75 | 15,826.05 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 5.40 | 5.73 | 13,851.00 | 14,697.45 |
| White Whole Cashews 450 | W450 | 5.07 | 5.29 | 13,004.55 | 13,568.85 |
| White Splits | WS | 3.75 | 3.97 | 9,618.75 | 10,183.05 |
| Large Pieces | LP | 2.98 | 3.42 | 7,643.70 | 8,772.30 |
| Small Pieces | SP | 1.65 | 2.21 | 4,232.25 | 5,668.65 |

**Chanzo:** Tanzania Association for Cashewnut Processors (TACP)

### 3.3 Bei ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje ya Nchi Hadi Kufikia Machi, 2024


Bei ya korosho karanga zinazobanguliwa na wabanguaji wa ndani na kuuzwa nje katika nchi za Uholanzi, Uturuki, Misri, nchi za Uarabuni, Marekani nk. Kuna mabadiliko kidogo ya bei kama inavyoonekana katika jedwali Na. 5

**Jedwali Na. 5: Bei ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje ya Nchi hadi kufikia Machi, 2024.**

| BEI YA KOROSHO KARANGA TANZANIA ZINAZOUZWA NJE HADI KUFIKIA MACHI, 2024 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | BEI DOLA/KILO (FOB) | | BEI TZS/KILO (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| WHITE WHOLE CASHEWS 180 | W180 | 7.80 | 8.15 | 20,007.00 | 20,904.75 |
| WHITE WHOLE CASHEWS 240 | W240 | 6.70 | 7.20 | 17,185.50 | 18,468.00 |
| WHITE WHOLE CASHEWS 320 | W320 | 6.05 | 6.80 | 15,518.25 | 17,442.00 |
| WHITE SPLITS | WS | 4.60 | 4.80 | 11,799.00 | 12,312.00 |
| LARGE WHITE PIECES | WS | 4.10 | 4.30 | 10,516.50 | 11,029.50 |

**Chanzo:** Tanzania Association for Cashewnut Processors **(TACP)**

**JEDWALI NAMBA 6: UWIANO WA BEI DARAJA WW320**




**Chanzo:** Bodi ya Korosho

## 4.0 MWENENDO WA ZAO LA KOROSHO NCHINI TANZANIA

Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2024 mauzo ya korosho ghafi kwa msimu wa 2023/2024 ni tani 271,396.965 zenye thamani ya shilingi 471,878,157,633.00 ambapo tani 244,796.965 zimekusanywa na kuuzwa katika ghala za minada zenye thamani ya shilingi 454,167,802,103.00. Mauzo ya korosho kupitia soko la awali hadi kufikia wiki ya mwisho ya mwezi Machi ni tani 8,330.335 zenye thamani ya shilingi 11,247,709,780.00 na korosho zilizobanguliwa na wabanguaji ni takribani tani 5,911.111 sawa na tani 26,600.00 za korosho ghafi zenye makadirio ya thamani ya shilingi 39,900,000,000.00. Ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji unaendelea.

Shughuli ya utoaji wa vibali vya kusafirisha Korosho ghafi nje ya nchi inaendelea ambapo hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2024 zaidi ya tani 242,173.336 za korosho ghafi zenye thamani ya Dola za Kimarekani 229,297,319.67 (FOB Value) zimepatiwa vibali vya kusafirisha nje ya nchi. Pia vibali vya kusafirisha Korosho karanga vinaendelea kutolewa na hadi sasa zaidi ya tani 1,804.212 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 9,111,818.47 (FOB Value) zimesafirishwa.

Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2024 jumla ya tani 219,087.94 sawa na asilimia 90.47 (90.47%) ya korosho zote zilizosafirishwa kwenda nchi za nje zimesafirishwa kupitia bandari ya Mtwara, tani 22,411.294 sawa na asilimia 9.25 (9.25%) za korosho zote zilizosafirishwa kwenda nje ya nchi zimesafirishwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam na tani 674.102 sawa na asilimia 0.28 (0.28%) za korosho zote zilizosafirishwa kupitia mpaka wa Horohoro-Tanga na kufanya jumla ya tani 242,173.336 zimesafirishwa kwenda nje ya nchi ambazo ni sawa na asilimia 91.73 (91.75%) ya mauzo ya korosho zote kupitia mfumo wa stakabadhi za ghala ambazo ni tani 244,796.965.

**Jedwali Na. 7b: Usafirishaji wa Korosho Karanga Tanzania Kwenda Nchi Mbalimbali Kuanzia Oktoba, 2023 hadi Machi, 2024.**

| USAFIRISHWAJI WA KOROSHO KARANGA KUTOKA TANZANIA KWENDA NCHI MBALIMBALI KUANZIA OKTOBA,2023 HADI MACHI, 2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **Na.** | **Nchi** | **Kiasi (Kg)** | **Thamani (USD FOB Value)** |
| 1 | Uholanzi | 809,676.00 | 4,440,342.00 |
| 2 | Kenya | 25,578.00 | 64,278.50 |
| 3 | Vietnam | 13,608.00 | 29,937.60 |
| 4 | Ubelgiji | 38,102.00 | 225,362.36 |
| 5 | China | 355,449.00 | 1,863,742.60 |
| 6 | Canada | 15,910.00 | 63,718.50 |
| 7 | Umoja wa Falme za Kiarabu | 127,000.00 | 677,132.20 |
| 8 | Uganda | 12,875.00 | 59,398.00 |
| 9 | Iraq | 2,500.00 | 11,310.00 |
| 10 | Kazakstan | 20,000.00 | 46,000.00 |
| 11 | Misri | 146,895.00 | 448,000.00 |
| 12 | Afrika Kusini | 29,361.56 | 126,205.44 |
| 13 | Lebanon | 14,564.00 | 20,000.00 |
| 14 | Uturuki | 24,969.80 | 151,824.46 |
| 15 | Iran | 99,900.00 | 484,337.00 |
| 16 | Kuwait | 15,000.00 | 15,000.00 |
| 17 | Omani | 13,100.00 | 13,100.00 |
| 18 | Saudi Arabia | 520.00 | 2,143.00 |
| 19 | Uswisi | 5,000.00 | 10,000.00 |
| 20 | Urusi | 28,800.00 | 147,889.00 |
| 21 | Marekani | 4,800.00 | 34,443.00 |
| 22 | Ujerumani | 905.00 | 8,619.00 |
| | **Jumla** | **1,804,513.36** | **8,942,782.66** |

**Chanzo:** Tanzania Association for Cashewnut Processors (TACP)

## JEDWALI NA. 7B: KOROSHO ZILIZOUZWA KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI GHALANI.

| Jumla ya Kiasi Kilichouzwa na Thamani (Novemba 21 hadi Novemba 30, 2023) | | |
|---|---|---|
| **KIPINDI CHA** | **KIASI KILICHOUZWA (MT)** | **THAMANI (TZS)** |
| Mwezi wa MACHI | NA | NA |
| Jumlishi Oktoba - MACHI | 244,796,965 | 454,167,802,103 |
| **JUMLA** | **244,796,965** | **454,167,802,103** |

## JEDWALI NA. 7C: MUHTASARI BEI ZA KOROSHO GHAFI KATIKA MINADA

| MUHTASARI BEI ZA KOROSHO GHAFI KATIKA MNADA | | | |
|---|---|---|---|
| **MWEZI ILIYOPITA (Februari,2024)** | | **MWEZI YA SASA (Machi, 2024)** | |
| **MWENENDO WA BEI** | **Mwezi** | **Daraja la Kawaida** | |
| | | **Bei ya Juu** | **Bei ya Chini** |
| | Bei ya Mwezi Machi | NA | NA |
| | Bei ya Mwezi Februari | 1,650 | 1,570 |
| | Mabadiliko (%) | | |

**UFUNGUO** “NA”= Haipo

**Jedwali Na. 7d: Bei za Mauzo ya Korosho Ghafi Kimkoa.**

| BEI YA MAUZO KOROSHO GHAFI YA MKOA (Machi, 2024) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MKOA** | **CHAMA KIKUU** | **MWEZI** | **DARAJA LA KAWAIDA** | |
| | | | BEI YA JUU | BEI YA CHINI |
| **MTWARA** | **MAMCU** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Januari | 1,300 | 1,250 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| | **MAMCU** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Januari | 1,510 | 1,500 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| **LINDI** | **RUNALI** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Januari | 1,650 | 1,550 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| | **LINDI MWAMBAO** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi januari | 1,560 | 1,500 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| **PWANI** | **CORECU** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Januari | 1,560 | 780 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| **RUVUMA** | **TAMCU** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Januari | 1,350 | 1,345 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| **MOROGORO** | **MOFACU** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Januari | 1,570 | 1,570 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |

**Ufunguo**: NA= Haipo
Chanzo: Bodi ya Korosho Tanzania

**Chanzo:** Bodi ya Korosho Tanzania

## 5.0 HALI YA UBORA WA KOROSHO MSIMU WA 2023/2024

Hali ya ubora kwa miaka 3 mfululizo imeendelea kuimarika kwa mujibu wa takwimu za mauzo ya korosho hadi kufikia tarehe 31/03/2024. Korosho daraja kwanza zilizoingia mnadani ni tani 240,852.707 ambazo ni sawa na asilimia 98.449 (98.449%) ya korosho zote zilizouzwa kwa njia ya mnada na korosho daraja la pili ni tani 3,793.319 ambazo ni sawa na asilimia 1.551 (1.551%) ya korosho zote zilizouzwa mnadani.

## 6.0 ZOEZI LA UHUISHAJI WA KANZIDATA YA WAKULIMA WA ZAO LA KOROSHO

Bodi ya korosho kwa kushirikiana na Halmashauri zinazolima zao la korosho inaendelea na zoezi la kuhuisha kanzi data ya wakulima wa korosho. Hadi kufikia mwezi Machi, 2024 tayari mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Pwani imehuisha kanzi data za wakulima. Zoezi bado linaendelea ambapo mpaka sasa jumla ya wakulima 441,029 tayari taarifa zao zimehuishwa ikiwa ni Pamoja na kutambua ukubwa wa mashamba yao (kuchukua coordinates), idadi ya mikorosho, picha za wakulima na taarifa zingine za muhimu kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 8. Aidha, Usajili wa Wakulima bado unaendelea.



## Jedwali Na. 8 Taarifa ya Mwenendo wa Uhuishaji wa Kanzidata ya Wakulima wa zao la Korosho.

| Na | Mkoa | Halmashauri | Idadi ya Wakulima Waliofikiwa |
|---|---|---|---|
| 1 | Mtwara | Manispaa ya Mtwara | 845 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara | 16,384 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba | 27,295 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba | 53,952 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Newala | 37,453 |
| | | Halmashauri ya Mji Newala | 23,382 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Masasi | 53,517 |
| | | Halmashauri ya Mji Masasi | 13,467 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu | 23,606 |
| 2 | Lindi | Manispaa ya Lindi | 10,762 |
| | | Halmashauri ya Mji Mtama | 26,230 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea | 27,233 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa | 27,231 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa | 7,340 |
| 3 | Ruvuma | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru | 64,392 |
| 4 | Pwani | Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti | 2,387 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga | 7,595 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji | 1,227 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo | 255 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze | 23 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha | 75 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Mafia | 55 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe | 684 |
| | | **Jumla** | **441,029** |

LIMETOLEWA NA
BODI YA KOROSHO TANZANIA

S.L.P 533
Mtwara
Simu (Bure) : 0 800 112 159
Nukushi : (023) 2333536
Barua Pepe: info@cashew.go.tz





MTWARA MAKAO MAKUU
www.cashew.go.tz


**#Ajenda10/30**